

Je mgongo kuuma kunasababishwa na nini?

Kama maumivu ya mgongo si kutokana na umri, au ugonjwa uliopo ndani ya mwili wako sasa, au si kutokana na ajali uliyoipata au hali uliyopo sasa kama Ujazito n.k?. Na umejaribu kutafuta kila suluhisho kwa madaktari bila mafanikio yoyote..basi fahamu kuwa huenda kuna ujumbe kutoka kwa Bwana unaopaswa kuujuua nyuma ya huo ugonjwa, na ukisha ujua na kuchukua hatua basi ugonjwa wako huo utaondoka mara moja.

Tusome maandiko yafuatayo..

Mithali 10:13 “Hekima hupatikana midomoni mwa mwenye ufahamu; Bali fimbo hufaa kwa mgongo wake asiye na ufahamu”

Mithali 19:29 “Hukumu zimewekwa tayari kwa wenye mzaha; Na mapigo kwa mgongo wa wapumbavu”

Mithali 26:3 “Mjeledi kwa farasi, Ijamu kwa punda, Na fimbo kwa

mgongo wa mpumbavu”.

Yatazame maisha yako je! Yamejaa mizaha?, yamejaa udunia? Je maneno yako yamejaa upumbavu?.. Kama hekima imepungua ndani yako, na mizaha imezidi katika maisha yako, basi huenda maumivu ya mgongo wako ni ujumbe kutoka kwa Mungu kwamba utubu na kugeuka. Na ukishatubu kwa kumaanisha kabisa kubadili njia zako, basi BWANA atakuponya mara moja!

Lakini kama njia zako na midomo yako ni ya hekima, basi fahamu kuwa ni mashambulizi umepokea kutoka kwa adui, lakini habari njema ni kwamba Yupo Mkuu wa uzima aliyeteswa kwaajili yetu, YESU KRISTO, mwombe huyo kwa Imani naye atakuponya kikabisa kabisa. Au wasiliana nasi kwa namba tajwa hapo chini, tuweze kukuombea kwa jina la Bwana Yesu Kristo naye atakuponya.

Maran atha!

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Tatizo la maumivu ya mgongo kibiblia.

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

Tatizo la Bawasiri kibiblia

Tatizo la kuvimba miguu kibiblia

TATIZO LA VISIGINO KUUMA KIBIBLIA

JE TATIZO LA KULA KUCHA NI ISHARA YA KUWA NA MAPEPO?

Chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu ndio kipi? (Matendo 21:25).

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp

Print this post